CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO CHUO KIKUU CHA DODOMA

(UDOM SACCOS LTD)

NAMBARI YA USAJILI:

PRI-DOM-DOM-CC-2022-130

SERA YA MFUKO WA MAEDELEO

Imeandaliwa na:
Bodi ya UDOM SACCOS LTD

TOLEO LA 1 , 2025

YALIYOMO

DIBAJI iii

TAFSIRI YA MANENO iv

SEHEMU YA KWANZA 1

UTANGULIZI 1

1.2 Mamlaka ya Kuandaa Sera hii 1

1.3 Lengo na Madhumuni ya Sera 2

SEHEMU YA PILI 3

UANZISHAJI WA MFUKO WA MAENDELEO 3

2.2 Uchangiaji wa Mfuko wa Maendeleo 3

SEHEMU YA TATU 5

USIMAMIZI WA MFUKO WA MAENDELEO 5

3.1 Kamati ya usimamizi wa mfuko 5

3.1.1 Muundo wa Kamati ya Usimamizi 5

3.1.2 Upatikanaji wa Kamati ya Usimamizi 5

3.1.3 Wajibu wa Kamati ya Usimamizi 5

3.2 Majukumu ya Bodi ya Chama 6

3.3 Matumizi ya Fedha za Mfuko 6

3.4 Utunzaji wa Hesabu za Mfuko 7

3.5 Taarifa za Hesabu za Mfuko 7

SEHEMU YA NNE 8

HITIMISHO 8

DIBAJI

Sera hii ya Uendeshaji wa Mifuko ya Maendeleo ni inaonesha shughuli nzima ya uanzishwaji, uendelezwaji na uhifadhi wa Mifuko ya maendeleo kwenye chama cha Ushirika wa akiba na mikopo cha chuo kikuu cha Dodoma, Miradi ya Pamoja ya Ushirika, Miradi ya Ubia na Shirikisho la Vyama vya Ushirika.

Sera hii imeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 142 (k) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika, ambacho kinafafanua taratibu za uanzishwaji, uchangiwaji, usimamizi, matumizi ya fedha za mfuko, sambamba na ukaguzi wake na uwasilishwaji wa taarifa za Hesabu za mfuko zilizokaguliwa kwenye Mikutano Mkuu na kuwasilishwa kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

Sera hii itasaidia chama katika upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo zikiwemo Uwekezaji katika maeneo mbalimbali, Masoko, manunuzi yenye kukidhi sifa na ubora n.k. Mifuko hii itasaidia kupata fedha kwa njia rahisi na gharama nafuu ikilinganishwa na vyanzo vingine vya fedha.

Aidha, sera hii itaisaidia Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mipango pamoja na shughuli za maendeleo zinazofanywa kwenye Vyama vya Ushirika na kuona namna zinavyomnufaisha Mwanachama, Chama cha Ushirika na Taifa kwa ujumla.

TAFSIRI YA MANENO

Kuanza kutumika kwa sera ya Uuzaji wa Mali za Chama

1 Sera hii itajulikana kama sera ya Uuzaji wa Mali za Chama na itaanza kutumika mara baada ya kupitishwa na kuidhinishwa na kusajiliwa na Mrajis.

Tafsiri

2 Katika sera hii, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo maneno yaliyoainishwa hapa chini yatakuwa na maana iliyotolewa:

a) "Afisa" maana yake ni mtu mwenye wadhifa wa kuchaguliwa au kuajiriwa katika Chama ambaye atajumuisha Meneja Mkuu, Mhasibu Mkuu, Mkaguzi wa Ndani, Mhazini na wengine waliopewa mamlaka chini ya sera hii ya chama;

b) "Mjumbe wa Bodi" maana yake ni mtu mwenye wadhifa wa kuchaguliwa au kuajiriwa katika Chama ambaye atajumuisha Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Bodi, Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi.

c) "Meneja" ni mtendaji mkuu wa Chama anayesimamia utendaji wa ujumla wa sera, matukio ya Chama na Bajeti na ni msemaji wa Chama kwa upande wa Menejimenti.

d) "Afisa Mikopo" itakuwa na maana ya mtu aliyeajiriwa na Chama kwa ajili ya kupitia na kuchambua maombi ya

mikopo yanayowasilishwa na wanachama na kufanya ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo hiyo;

e) "Sheria" ni mfumo wa kanuni ambazo hutekelezwa na taasisi maalumukatika Nyanja ya siasa, uchumi, na jamii kwa njia mbalimbali na huratibu mahusiano baina ya watu. Mifumo ya sheria inaeleza haki na wajibu wa kila mmoja.

f) " "Mrajis Msaidizi" ni kiongozi wa vyama vya ushirika Mkoa anayeteuliwa na Mrajis wa taifa wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa ajili ya kuongoza ushirika katika Mkoa;

g) "Bodi ya Uongozi" maana yake ni chombo kilichochaguliwa na wanachama kupitia Mkutano Mkuu kwa ajili ya kusimamia shughuli za kila siku za chama;

h) "Chama" maana yake ni Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha UDOM SACCOS LTD kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika;

i) ""Dhamana" ni kitu chochote ambacho mtu anaweka au kuwekewa ili kukomboa kitu fulani au kupata huduma fulani. Dhamana inaweza kuwa fedha, gari, nyumba na hata chochote kile;

j) "Mkataba" ni makubaliano ya kisheria kati ya watu wawili au zaidi au wahusika ambapo katika sera hii ni baina ya mkopeshaji au mkusanya madeni na mkopaji.

k) "Mdhamini" maana yake ni mwanachama anayemchukulia mwanachama mwingine dhamana kuwa atatimiza jambo fulani;

l) "Adhabu" maana yake ni fedha analolipa mwanachama kwa kutorejesha marejesho ya mkopo kwa muda uliopangwa;

m) "Mrajis" maana yake ni kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013;

n) "Sera/Mwongozo" maana yake ni utaratibu uliowekwa na wanachama kuongoza watendaji wa Chama katika uendeshaji wa shughuli za chama ili kufikia malengo yaliyowekwa kwa manufaa ya wanachama;

o) "Sheria" ina maana ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 pamoja na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na. 10 ya Mwaka 2018;

p) "Tume" ina maana Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC);

q) "Mali" ni chochote kinachoweza kumilikiwa na Chama kinaweza kuhamishika au kisichoweza kuhamishika;

r) "Kibali" ni idhini inayotolewa na Mamlaka husika kwa ajili ya kuzingatia utaratibu wa kiutendaji.

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

Sera ya uendeshaji wa mifuko ya maendeleo ni nyenzo inayotoa maelekezo ya namna ya kuanzisha na kuendesha mifuko ya maendeleo katika chama; kwa malengo ya kugharimia shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwa ni pamoja na Uwekezaji katika maeneo mbalimbali, Masoko, ununuzi n.k. Sera hii imeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 142(k) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013.

Kumekuwa na changamoto mbalimbali kwenye uanzishwaji wa Mifuko ya Maendeleo kwenye Vyama vya Ushirika. Changamoto hizo ni pamoja na: Vyama kuanzisha mifuko isiyokuwa na utaratibu maalum; shughuli za mifuko kuingiliana na shughuli za kawaida za chama; mifuko inayoanzishwa kukosa usimamizi madhubuti na kufanya matumizi kinyume na malengo yaliyokusudiwa n.k.

Ili kutatua changamoto hizo, sera hii imeainisha mambo muhimu ya kuzingatia kabla na baada ya kuanzisha mfuko wa maendeleo, ili kufikia malengo tarajiwa na kuepusha matumizi mabaya ya fedha za mfuko. Sera hii imeandaliwa kwa lengo la kuweka uelewa wa pamoja kwenye chama wakati wa uanzishaji wa mifuko na baada ya kuanzisha mifuko kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake.

Sera hii inatoa maelekezo mahsusi kwa ajili ya Bodi ya UDOM SACCOS LTD, Wanachama na watendaji kuhusu namna ya uanzishwaji na uendeshwaji wa mifuko ya maendeleo ndani ya chama, baada ya kuonekana kuwa baadhi ya vyama vimekuwa vikianzisha mifuko hii bila kuwa na utaratibu maalum wa namna ya kuiendesha.

1.2 Mamlaka ya Kuandaa Sera hii

Sera hii imeandaliwa na Bodi ya UDOM SACCOS LTD kwa kuzingatia kifungu cha 141 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013, na Kanuni ya 81 ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015.

1.3 Lengo na Madhumuni ya Sera

1.3.1 Lengo kuu

Lengo la Sera hii ni kuweka utaratibu utakaosaidia katika uanzishwaji na usimamizi wa mifuko ya maendeleo katika Chama cha UDOM SACCOS LTD kwa ufanisi kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na taratibu za uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika na Sheria nyingine za Nchi.

1.3.2 Madhumuni

Madhumuni ya sera hii ni pamoja na:

(i) Kutoa utaratibu wa uanzishwaji na usimamizi wa mifuko ya maendeleo katika Chama;

(ii) Kuainisha malengo ya uanzishwaji wa mifuko ya maendeleo katika Chama; na

(iii) Kutoa maelekezo ya namna ya kukusanya fedha za mfuko.

1.4 Walengwa wa Sera hii

Sera hii imeandaliwa kwa ajili ya kutumiwa na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) Maafisa Ushirika;

(ii) Wanachama, Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika;

(iii) Watendaji na viongozi wa Wizara za Kisekta, Mamlaka za Serikali, na taasisi mbalimbali za umma zinazofanya kazi na Vyama vya Ushirika; na

(iv) Wadau wengine wa maendeleo.

SEHEMU YA PILI

UANZISHAJI WA MFUKO WA MAENDELEO

Chama kinaweza kuanzisha mfuko wa maendeleo kutegemeana na mahitaji. Ili kuhakikisha kuwa mahitaji yaliyokusudiwa yanafikiwa, chama kinatakiwa kuzingatia taratibu wakati wa uanzishaji na uchangiaji wa mifuko hiyo kwa kuzingatia: taratibu za uanzishaji wa mfuko; na uchangiaji wa mfuko wa maendeleo.

2.1 Taratibu za Uanzishaji wa Mfuko

Uanzishwaji wa mfuko wa maendeleo katika chama utasimamiwa na Bodi ya chama ambapo itapaswa kuzingatia taratibu zifuatazo:

(i) Kufanya upembuzi utakaobainisha mahitaji na kuandaa mapendekezo ya kuanzishwa kwa mfuko;

(ii) Kupeleka mapendekezo kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kujadiliwa na kuazimia uanzishaji wa mfuko;

(iii) Endapo Mkutano Mkuu utapitisha mapendekezo hayo, Bodi ya chama itaandaa andiko kwa ajili ya uanzishwaji wa mfuko; na kisha

(iv) Kuwasilisha andiko la mfuko kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika kwa ajili ya kuidhinishwa.

2.2 Uchangiaji wa Mfuko wa Maendeleo

Uchangiaji wa mfuko wa maendeleo utategemeana na aina na mahitaji ya chama. Utaratibu wa uchangiaji wa mfuko wa maendeleo utakuwa kama ifuatavyo:

(i) (a) Maamuzi ya namna ya kuchangia mfuko yatafanywa na wanachama katika Mkutano Mkuu;

(b) Chama hakitaruhusiwa kukusanya fedha pasipo ridhaa ya wanachama kwa kupitia Mkutano Mkuu**;**

(ii) Wanachama watajadili chanzo cha fedha, kiwango na muda watakaochangia kwenye mfuko kwa kuzingatia malengo ya uanzishwaji wa mfuko;

(iii) Fedha za mfuko zitachangwa kwa utaratibu uliokubaliwa kwenye Mkutano Mkuu ikiwa ni pamoja na mwanachama kuchangia fedha taslimu, kukatwa kwenye kwenye akiba/huduma nyingine; na

(iv) Fedha zilizochangwa kwenye mfuko hazitarudishwa kwa mwanachama, bali zitatumika kwa ajili ya malengo mahsusi yaliyoainishwa kwenye andiko la mfuko. Mwanachama atanufaika na mapato yatakayotokana na mfuko kwa kuzingatia uwiano wa kile alichochangia.

TANBIHI: Ni muhimu ikazingatiwa kwamba utaratibu wa makato kwa ajili ya shughuli za uanzishaji na uendeshaji wa mfuko hazitaongeza gharama za huduma kwa mwanachama

Mfuko utaendeshwa kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa; hivyo, hautahusika katika kugharamia shughuli nyingine yoyote ambayo haikuwa kwenye lengo la uanzishwaji wake pasipo kupata idhini ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

SEHEMU YA TATU

USIMAMIZI WA MFUKO WA MAENDELEO

Ili kuondoa mwingiliano wa shughuli zake na zile za msingi za chama ikiwa ni pamoja na kuleta ufanisi na kuimarisha udhibiti wa shughuli za maendeleo ndani ya chama mfuko hauna budi kuwa na uongozi unaojitegemea. Chama kitaunda kamati ambayo itakuwa na wajibu wa kusimamia shughuli za mfuko. Kamati hii itajulikana kama Kamati ya Usimamizi wa Mfuko.

3.1 Kamati ya usimamizi wa mfuko

Bila kuathiri majukumu ya kawaida ya Bodi ya Chama, Kamati ya Usimamizi wa Mfuko itafanya kazi zake za usimamizi wa shughuli zote za mfuko wa maendeleo kwa mujibu wa majukumu kama yalivyoainishwa kwenye sera hii.

3.1.1 Muundo wa Kamati ya Usimamizi

Kamati ya Usimamizi itaundwa na:

(i) Wajumbe wasiopungua wawili (2) ambao watatokana na wajumbe wa Bodi;

(ii) Mjumbe mmoja (1) kutoka nje ya Bodi ambaye atatakiwa kuwa na utaalam wa shughuli inayotarajiwa kufanyika; na

(iii) Mtendaji maalum kwa ajili ya kutunza vitabu na kumbukumbu zote za Mfuko.

3.1.2 Upatikanaji wa Kamati ya Usimamizi

Bodi ya Chama itapeleka mependekezo ya Wajumbe kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kuidhinishwa.

3.1.3 Wajibu wa Kamati ya Usimamizi

Kamati ya Usimamizi wa Mfuko itakuwa na Wajibu kama ifuatavyo:

(i) Kutoa mapendekezo kwenye Bodi kuhusu uendeshaji wa Mfuko;

(ii) Kuhamasisha uchangiaji wa mfuko na kuchukua hatua kwa mwanachama atakayekaidi maamuzi ya Mkutano Mkuu juu ya

uchangiaji wa mfuko wa maendeleo kwa kushirikiana na Bodi ya Chama;

(iii) Kutoa taarifa za uendeshaji wa mfuko katika vikao vya Bodi, Mkutano Mkuu wa Chama na katika ofisi ya Mrajis wa vyama vya Ushirika pale itakapohitajika;

(iv) Kusimamia rasilimali zote za mfuko, kwa kushirikiana na Bodi; na

(v) Kutekeleza shughuli zozote zile kwa ajili ya manufaa na maendeleo mfuko.

3.2 Majukumu ya Bodi ya Chama

Bodi, kama Msimamizi Mkuu wa shughuli za Chama, itatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Masharti ya Chama. Kwa upande wa Mfuko wa Maendeleo wa Chama, Bodi itakuwa na majukumu yafuatayo:

(i) Kuhakikisha kuwa Kamati ya Usimamizi wa Mfuko inatekeleza majukumu yake;

(ii) Kuhakikisha kuwa Kamati ya usimamizi inaandaa na kutunza taarifa za Mfuko;

(iii) Kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za mfuko; na

(iv) Kuhakikisha kuwa malengo ya uanzishwaji wa Mfuko yanafikiwa.

Tahbihi:

(i) Pale ambapo Bodi itaona kuwa Kamati ya Usimamizi imeshindwa kutekeleza majukumu yake, itapeleka mapendekezo kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya maamuzi.

(ii) Kutapokuwa na viashiria vya hatari katika uendeshwaji wa Mfuko, Mrajis wa Vyama vya Ushirika ataweza kuchukua hatua wakati wowote.

3.3 Matumizi ya Fedha za Mfuko

Matumizi yoyote za fedha za Mfuko yatafanyika kwa kuzingatia madhumuni yaliyoainishwa kwenye andiko la Mfuko. Ili kuimarisha udhibiti wa uendeshaji wa mfuko huo mambo yafuatayo yatatakiwa kuzingatiwa:

(i) Matumizi yoyote ya mfuko wa maendeleo ya chama yatafanyika baada ya kuwa yamepitishwa kwenye Mkutano Mkuu na kuidhinishwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika;

(ii) Fedha za Mfuko zitakazohusu manunuzi zitatumika kwa kuzingatia taratibu za manunuzi zilizoelezwa kwenye sera/kanuni za manunuzi ya chama; na

(iii) Kufanya malipo ya fedha kwa mujibu wa taratibu za Kihasibu.

3.4 Utunzaji wa Hesabu za Mfuko

Ili kuhakikisha kuwa hakuna muingiliano wa fedha za chama, yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:

(i) Fedha za mfuko wa maendeleo zinapaswa kuwa na vitabu vyake maalum kwa ajili ya miamala ambayo hesabu zake zitaandikwa na kutunzwa kikamilifu;

(ii) Fedha za mfuko zitajitegemea na zitatakiwa kutunzwa katika akaunti maalum inayojitegemea;

(iii) Matumizi ya fedha za mfuko yatakaguliwa kwa utaratibu wa kawaida wa ukaguzi wa hesabu za chama. Mrajis wa Vyama vya Ushirika atakagua shughuli za mfuko wakati wowote kwa jinsi atakavyoona inafaa; na

(iv) Mkaguzi wa nje anayekagua hesabu za chama ndiye atayekagua hesabu za mfuko na taarifa yake itapelekwa kwenye Vikao vya Bodi, Mkutano Mkuu na katika ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

3.5 Taarifa za Hesabu za Mfuko

(i) Taarifa za hesabu za mfuko zitawasilishwa katika vikao vya Bodi, na kisha kupelekwa kwenye Mkutano Mkuu ili wanachama waweze kujua mwenendo wa uendeshaji wa mfuko; na

(ii) Taarifa za fedha za mfuko zitaingizwa kwenye vitabu vya hesabu kwa utaratibu wa kawaida wa utunzaji wa hesabu za chama. Taarifa zinazopaswa kuandaliwa ni pamoja na;

a) Taarifa ya makusanyo ya fedha za Mfuko;
b) Matumizi yaliyofanyika kupitia fedha za mfuko kulingana na bajeti iliyoidhinishwa, na
c) Taarifa ya jumla ya mapato na matumizi ya fedha za mfuko.

SEHEMU YA NNE

HITIMISHO

Mifuko ya maendeleo katika Chama itachangia katika maendeleo tarajiwa endapo itatumika kwa kuzingatia madhumuni ya uanzishwaji wake. Sera hii itasaidia kutatua changamoto zilizopo katika uanzishaji, uendeshaji na usimamizi wa Mifuko hii muhimu katika chama iwapo kila Mdau atatekeleza wajibu wake.

Vilevile, utekelezaji wa sera hii itaisaida chama kutatua changamoto mbalimbali zinaotokana na mifuko ya maendeleo. Kwa kutumia sera hii, Mrajis wa Vyama vya Ushirika, Bodi ya Chama, Maafisa Ushrika na wanachama watakuwa na nafasi nzuri ya kusimamia Mifuko hii ili iweze kuwa na tija na kukisaidia chama cha UDOM SACCOS LTD kuondokana na utegemezi kutoka kwenye Taasisi mbalimbali za kifedha.

Sera hii itafanyiwa maboresho (marekebisho) mara kwa mara ili kurekebisha, kuongeza jambo pale itakapoonekana kuwa inalazimu kufanya hivyo kwa maslahi ya wanachama kadiri ya Bodi na Mkutano Mkuu itakavyoonesha inafaa. Maboresho yoyote yatafanyika kwa kuzingatia sheria ya Vyama vya ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na kanuni za SACCOS 2015.

Sera hii imetayarishwa na Bodi ya UDOM SACCOS LTD na baada ya kukasimishwa mamlaka ya Mkutano Mkuu wa Chama na Ofisi ya Mrajis mkoa Dodoma ya uhuishaji wa sera kutokana na miongozo iliyotolewa na ofisi ya Mrajis Taifa ya mwaka 2022 ya 11/3/2024 na itaanza kutumika baada ya kuidhinishwa na Mrajis.

_____

Mrajis Msaidizi (M) Dodoma

Tarehe_____